# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA NANE

**04 SEPTEMBA, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 04 SEPTEMBA, 2026

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**102. MHESHIMIWA SHEILA EDWARD LUKUBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itachukua deni la ujenzi wa Stendi ya Msamvu ili kuipunguzia mzigo Manispaa ya Morogoro.

**103. MHESHIMIWA CHIKU ATHMAN ISSA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni kuwa sababu ya kutokuwa na matokeo makubwa ya Mikopo ya 10% ni kukosekana Wataalam wa Mafunzo ya biashara.

**104. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya Kata ya Nyanzenda na Maisome Jimbo la Buchosa.

**105. MHESHIMIWA MARTHA NEHEMIA GWAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Makanda-Manyoni Mashariki utaanza.

**OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):**

**106. MHESHIMIWA HALIMA ABDALLAH BULEMBO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuanzisha *Youth Investment Resources Centre* kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya 2007.

**107. MHESHIMIWA ZULFA MMAKA OMARY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, kuna mikakati gani kuhakikisha kuwa ajira na uwezeshaji wa Vijana haziishii kwenye Programu za mafunzo pekee bali uzalishaji wa ajira halisi.

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

**108. MHESHIMIWA HIJA HASSAN HIJA (KIWANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuwawezesha Wananchi kuongeza wigo wa kufanya biashara ya Hewa Ukaa (*carbon*).

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**109. MHESHIMIWA SALUM KHAMIS SALIM (BUBUBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali inampango gani wa kutoa elimu kwa Wafugaji pamoja na kuongeza maeneo ya malisho yanayolingana na idadi ya Mifugo.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**110. MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali imejipangaje kuchakata na kuleta Bungeni Mabadiliko ya Sheria ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**111. MHESHIMIWA ALI KHALIL MIRZA (KIEMBE SAMAKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni haja ya kujenga Kituo cha Polisi cha Daraja B Wadi ya Shakani ili kuimarisha usalama kuelekea Mashindano ya AFCON 2027.

**WIZARA YA UJENZI:**

**112. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kuna hatua gani za haraka kuwaondolea Wananchi kero inayotokana na kutumia Barabara ya Makambako – Songea ambayo imechakaa.

**113. MHESHIMIWA ZAINAB RASHID KAWAWA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Liwale – Nangurukuru yenye Kilometa 231 kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA KILIMO:**

**114. MHESHIMIWA MECKTRIDIS FRATERN MDAKU (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutekeleza Mradi wa Umwagiliaji katika maeneo ya Mkasisi, Usangule na Sofi – Malinyi.

**115. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaweka Ruzuku kwenye bei ya Mbegu Bora kama ilivyofanya kwenye bei ya Mbolea.

**WIZARA YA MAJI:**

**116. MHESHIMIWA KIJAKAZI YUNUS MOHAMED (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutatua kero ya maji katika Kata ya Lihimalyao Kilwa wakati wakisubiri upanuzi wa Mradi wa Pande *Plot*.

**117. MHESHIMIWA ADONIS ALFRED BITEGEKO (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Miradi miwili ya Maji ya Makongora na Iroba katika Jimbo la Muleba Kaskazini ili kutatua tatizo kubwa la maji.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**118. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha *academy* maalum ili kuibua vipaji kwa Watoto kutoka mashuleni.

**WIZARA YA FEDHA:**

**119. MHESHIMIWA YANNICK IKAYO NDOINYO (NGORONGORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Forodha maeneo ya mpakani katika Tarafa za Loliondo na Sale Wilayani Ngorongoro.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**120. MHESHIMIWA TINNAR ANDREW CHENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, kwanini Wananchi wanatozwa Riba ya Pango la Ardhi Januari hadi Juni badala ya kuanza kutozwa unapoanza Mwaka Mpya wa Fedha wa Serikali.

**WIZARA YA MADINI:**

**121. MHESHIMIWA SALEHE MBWANA MHANDO (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Ofisi ya Madini Wilayani Kilindi.

## III. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

## IV. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

**WAZIRI MKUU:**

## V. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI:

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **04 SEPTEMBA, 2026** | **KATIBU WA BUNGE** |